# Ujitokezaji wa Viambishi Njeo na Athari zake Kifonolojia katika Lugha za Kibantu: Mifano kutoka Lugha ya Shimalila

Pendo Mwashota

## Ikisiri

Makala hii inajadili kuhusu ujitokezaji wa viambishi njeo na athari zake kifonolojia katika lugha za Kibantu. Mifano iliyotumika ni ya lugha ya Shimalila kutoka nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Guthrie (1948), Shimalila ipo katika ukanda wa M 20. Lugha nyingine zilizopo katika ukanda huu ni kama vile Wanda, Mwanga, Kisafwa, Iwa, na Tambo. Kuna vipengele vingi vya kiisimu ambavyo havijafanyiwa uchunguzi katika lugha ya Shimalila. Kwa mfano, vipengele vya kifonolojia, kisintaksia, kimofolojia, kisemantiki na vinginevyo. Pamoja na kuwapo kwa vipengele tajwa kutofanyiwa uchunguzi makala hii inajadili kipengele kimoja cha kimofolojia yaani, viambishi njeo tu. Katika kujadili kipengele hicho cha kiisimu imebainika kuwa lugha ya Shimalila ina ujitokezaji wa pekee wa viambishi njeo vya wakati uliopita tofauti na ilivyo katika lugha ya Kiswahili[1]. Yaani, katika Shimalila kuna viambishi njeo vya wakati vinavyojitokeza kabla ya mzizi wa shina na vingine vinavyojitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Vilevile Makala inaonesha kuwa wakati mwingine upachikaji wa viambishi njeo katika lugha ya Shimalila huhusisha taaluma ya mofolojia na fonolojia. Chanzo cha data za utafiti huu ni vitabu mbalimbali vinavyohusu lugha ya Shimalila, navyo vimeandikwa na watu mbalimbali wa jamii ya Shimalila ambao malengo yao ni kutafsiri Biblia kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Shimalila. Pia, data nyingine zimetokana na hojaji pamoja na usaili wa moja kwa moja wa wazungumzaji watano wa lugha ya Shimalila.

## 1.0 Utangulizi

Viambishi njeo ni kipengele cha kiisimu kilichozungumziwa na wanaisimu mbalimbali kwa kiasi kidogo. Hata hivyo, baadhi ya wanaisimu kama vile Mgullu (1999), Habwe na Karanja (2007), Matei (2008), Waihiga (2010) na Chomi (2012) wamezungumzia viambishi njeo katika lugha ya Kiswahili kwa kuvitaja na kuvibainisha. Wanaisimu hao hawajaeleza athari za kifonolojia zinazoweza kujitokeza wakati wa upachikaji wa viambishi vya njeo katika mizizi ya vitenzi. Kutokana na ukosefu wa data zinazoelezea suala la athari za kifonolojia zinazoweza kujitokeza katika viambishi njeo vya lugha za Kibantu, makala hii

[1] Lugha ya Kiswahili imetumika kwa sababu ni lugha ambayo imefanyiwa utafiti wa kiisimu kwa kiwango kikubwa tofauti na lugha nyingine za Kibantu.

inajadili suala hilo kwa kina kwa kutumia mifano kutoka katika lugha ya Shimalila. Shimalila ni lugha inayozungumzwa na Wamalila wanaopatikana katika mkoa wa Mbeya hasa upande wa Mbeya Vijijini katika tarafa ya Isangati. Mbali na Isangati, wazungumzaji wa Shimalila wanapatikana pia katika maeneo ya Mbalizi, Sumbawanga na Mbozi kwa kiasi kidogo. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu taarifa tangulizi ambapo kuna fasili ya dhana zilizotumika katika makala nazo ni maana ya viambishi, viambishi njeo, aina za viambishi njeo, na maana ya vitenzi. Sehemu ya pili inahusu viambishi njeo katika lugha ya Shimalila ambapo kuna ufafanuzi wa aina tatu za viambishi njeo katika Shimalila. Viambishi njeo vilivyofafanuliwa ni kiambishi njeo cha wakati uliopo, kiambishi njeo cha wakati uliopita na kiambishi njeo cha wakati ujao katika lugha ya Shimalila. Sehemu ya tatu ambayo ni ya mwisho inahusu hitimisho la makala. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali, yaani vile udurusu wa maandiko maktabani, hojaji na usaili. Kabla ya kuangalia kiundani kuhusu viambishi njeo katika lugha ya Shimalila sehemu inayofuata inafafanua kwa ufupi dhana za msingi zilizotumika katika makala hii ambazo ni viambishi, viambishi njeo na vitenzi.

### 1.1 Maana ya Viambishi

Viambishi hurejelewa kwa istilahi tofautitofauti kutegemeana na uga wa taaluma inaozungumziwa. Hii ina maana ya kwamba wakati mwingine mofimu pia huweza kuitwa viambishi hususani mofimu tegemezi. Katika sehemu hii maana iliyokusudiwa ni kusema kuwa wakati mwingine mofimu huweza kuitwa viambishi. Pia, viambishi katika muktadha mwingine wa kisarufi hujulikana kama mofu. Wakati mwingine viambishi huweza kuitwa alomofu kulingana na mazingira ya utokeaji wake. Baada ya kuangalia istilahi mbalimbali zinazorejelea viambishi, hebu tuangalie fasili ya viambishi kwa mujibu wa wanaisimu mbalimbali.

Kwa mujibu wa Matei (2008:95) kiambishi ni neno linalotokana na ‘uambishaji’ au ‘kuambisha.’ Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa uambishaji ni ule utaratibu wa kuongeza viambishi katika mzizi wa neno. Kiambishi ni sehemu (mofu) ambayo huambikwa kwenye mzizi wa neno ili kulipa maana ya ziada. Matei anafafanua kuwa kiambishi kinaweza kubadilisha kategoria ya neno ama huweza kulipa neno maana au hali ya ziada tu bila kubadilisha aina ya neno hilo. Kwa upande wake Waihiga (2010:115) anasema kuwa katika lugha za Kibantu, ni muhimu sana kuelewa vitenzi na viambishi vyake kwa sababu maana kamili ya kitenzi hutegemea viambishi vinavyokipamba kitenzi husika. Hii ina maana ya kwamba ndani ya kitenzi cha lugha za Kibantu kuna viambishi mbalimbali vinavyoambatana na mzizi wa kitenzi. Viambishi hivyo huwa na uamilifu tofautitofauti kulingana na nafasi ya ujitokezaji wake katika mzizi wa kitenzi.

Katika makala hii viambishi ni visehemu vya neno vinavyoambikwa mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno ili kujaziliza maana ya neno kulingana na kaida za lugha husika.

Kuhusiana na viambishi njeo wanazuoni mbalimbali wamejaribu kueleza juu ya viambishi hivyo. Hata hivyo, mapitio ya maandiko mbalimbali yanaonesha kuwa wanazuoni wengi wamechunguza zaidi viambishi njeo katika lugha ya Kiswahili (taz. TUKI, 1990; Matei, 2008:99; Waihiga, 2010:118; Chomi, 2012:41). Hakuna data zozote zinazoonesha namna wanazuoni walivyozungumzia viambishi njeo katika lugha ya Shimalila.

## 1.2 Viambishi Njeo

Kwa mujibu wa TUKI (1990) njeo ni kategoria ya kisarufi ambayo huwakilisha muda au wakati tendo hufanyika/linapofanyika. Pia, kiambishi njeo huwa ni kiambishi awali kinachomaanisha kuwa mofimu hii huja kabla ya mzizi wa kitenzi. Naye Waihiga (2010:99) anaeleza kuwa, viambishi vya wakati/njeo huambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi kuonesha wakati wa kutendeka kwa kitendo/jambo. Kwa ujumla viambishi njeo ni visehemu vya neno vinavyoweza kupachikwa mwanzoni, katikati au mwishoni mwa mzizi wa kitenzi kulingana na taratibu za lugha husika.

### 1.2.1 Aina za Viambishi Njeo

Habwe na Karanja (2007:103) wanasema kuwa kuna aina tatu za njeo, nazo ni njeo ya wakati wa sasa, wakati uliopita, na wakati ujao. Waihiga (2010:118) anaeleza kuwa kuna nyakati za aina tatu zinazowakilishwa na viambishi mbalimbali katika Kiswahili yaani, wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao. Aidha, wanazuoni wengi wa isimu ya Kiswahili kama vile Mgullu (1999), Massamba na wenzake (2001), Habwe na Karanja (2007), Matei (2008), Waihiga (2010), Chomi (2012), na Matinde (2012) wanakubaliana kuwa wakati uliopo huwakilishwa na kiambishi ‘-na-’, wakati uliopita huwakilishwa na kiambishi ‘-li-’ na wakati ujao huwakilishwa na kiambishi ‘-ta-’. Njeo ni miongoni mwa kategoria za kisarufi zinazosaidia kufasili dhana ya kitenzi. Katika makala hii tumeungana na mawazo yaliyotolewa na wanazuoni waliofafanua aina za njeo. Hii inatokana na ukweli kwamba njeo zilizozungumziwa ni za namna tatu na si vinginevyo. Njeo ya wakati uliopita timilifu imetumika katika udondozi wa kuielezea njeo ya wakati uliopita katika Shimalila kwa sababu kimofolojia inafanana na namna inavyoandikwa njeo ya wakati uliopita tofauti ipo katika matamshi.

## 1.3 Maana ya Vitenzi

Dhana ya vitenzi imeelezwa na wanazuoni tofautitofauti kama ifuatavyo: Richard na wenzake (1985) wanasema kuwa kitenzi ni neno ambalo hutokea kama sehemu muhimu ya kiarifu na ambalo huambishwa mofu za njeo, hali, nafsi, idadi na

dhamira. Aidha, vitenzi hueleza juu ya tendo au hali. Naye Nkwera (2003:2) anasema kuwa vitenzi ni maneno yanayoarifu jambo ambalo hufanywa na jina au kufanyiwa jina. Pia, Nkwera anaeleza kuwa kitenzi kinaweza kuwa kiwakilishi au kivumishi kisimamapo peke yake kama jina. Vitenzi hutaja matendo, matukio, hali au mabadiliko. Kitenzi ni neno ambalo limebebeshwa vitu vingi ndani yake suala linalowafanya wanasarufi wengi kupendelea kuliita neno hilo kifungutenzi badala ya kitenzi.

Naye Mdee (2007:33) anatoa maana ya kitenzi kuwa ni neno linaloeleza jambo linalotendwa na lililotendeka. Kitenzi huarifu tendo lililofanywa au litakalofanywa na mnyama, mtu, au kiumbe chochote kinachoweza kutenda jambo. Mdee anaendelea kufafanua kuwa vitenzi vya Kiswahili havisimami pekee vinapotumiwa katika tungo, bali huambatana na viambishi vingine vyenye kuwakilisha mtenda wa tendo au mtendewa wa jambo. Kitenzi huambatishiwa pia viambishi vyenye kuonesha wakati tendo linapofanyika, kama mfano ufuatao unavyoonesha:

**Mfano wa 1:**

Dada a-na-soma Watoto wa-na-ruka Baba a-ta-fika

Mgullu (2010:182) anasema kuwa vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu sana ya kiarifu cha sentensi ambayo hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ni maneno pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ndipo kifungu cha maneno kiweze kuwa sentensi, Kwa mfano katika sentensi: Mtoto anakula. Aidha, Matinde (2012:150) anaeleza kuwa kitenzi ni neno linalotoa taarifa kuhusu tendo lililofanyika, linalofanyika au litakalofanyika. Katika muundo msingi wa tungo za Kiswahili kitenzi ndilo neno kuu katika sehemu ya kiarifu au kirai tenzi. Kitenzi kinapoondolewa katika sentensi bila shaka kifungu hicho cha maneno hukosa maana. Matinde anafafanua kuwa vitenzi huweza kusimama bila msaada wa aina zingine za maneno na sentensi ikawa kamilifu na yenye uarifishaji mkamilifu.

Kwa upande wake, Matei (2008:66) anafafanua mambo ambayo vitenzi huarifu nayo ni kama yafuatayo:

i. Kinachotendwa au kinachotendeka kwa nomino.
ii. Nomino ni nini? Ni ya aina au tabia gani? Kwa mfano: Ukuta huo ni mrefu.
iii. Hali ya kuwa na, kwa mfano:
  Hawa hawana adabu.
  Wacha Mungu wana utu.
iv. Hali ya vitenzi vya aina hii hueleza hali fulani badala ya tendo. Kwa mfano:

Julia aliamini kwamba angepita mtihani.
Nadhani nchi yetu imeanza kudumisha demokrasia.

Viambishi hubebwa kwa kiwango kikubwa katika vitenzi kuliko ilivyo katika aina zingine zote za maneno ya Kiswahili. Vitenzi vya Kiswahili huwa vina sehemu kuu tatu: viambishi awali, mzizi wa kitenzi, na viambishi tamati. Hata hivyo si kusudi la makala hii kujadili sehemu kuu za viambishi vya vitenzi katika lugha yoyote ile. Kama ilivyoelezwa awali kwamba makala hii inajadili viambishi njeo vya vitenzi vya Shimalila. Itakuwa si jambo la busara kiisimu kujikita tu katika viambishi njeo bila kutaja aina nyingine za viambishi awali katika vitenzi. Katika vitenzi kuna viambishi awali vifuatavyo: Viambishi vya nafsi kwa mfano viambishi vya nafsi ya kwanza umoja 'ni-' na 'tu-' katika wingi, Viambishi vya njeo kwa mfano '-na-' katika wakati uliopo, '-li-' katika wakati uliopita na '-ta-' katika wakati ujao, viambishi vipatanishi/ngeli kwa mfano 'm-/mu-', 'wa-' ngeli ya kwanza, viambishi vya masharti kwa mfano '-nge-', '-ngeli-', '-ngali-', na '-ki-', viambishi vya urejeshi kwa mfano '-ye-', na '-o-', viambishi vya kujitendea kwa mfano, '-ji-', viambishi vya yambwa kwa mfano 'ali-**mu**-andikia' na viambishi fuatishi kwa mfano 'alipig-**ish**-a'. Makala hii inahusu viambishi njeo, aina zingine za viambishi vimetolewa kutoka katika lugha ya Kiswahili kwa ajili ya mifano na msisitizo. Aidha, ijulikane kwamba viambishi tajwa kutoka katika lugha ya Shimalila imeanza kufafanuliwa kuanzia katika sehemu ya 2 ya makala hii.

### 1.4 Njeo katika Lugha nyingine za Kibantu

Kuna wanazuoni mbalimbali waliozungumzia suala la njeo katika lugha za Kibantu. Miongoni mwa wanazuoni hao ni Besha (1989), Muzale (1998), Mreta (1998), Nurse (2003), Lusekelo (2007), Mpalanzi (2010), Cosmas (2010), Kanijo (2012) na Nyinondi (2013) kwa kuwataja wachache. Katika kazi zao wameelezea zaidi kuhusu njeo na hali na namna zinavyojitokeza kimofolojia. Kwa mfano, katika lugha ya Kinyakyusa Lusekelo amebainisha viambishi vya njeo ya wakati uliopo ambavyo ni -ku-….-a, wakati uliopita ni -ø-….-ile na -a-…-ile, na viambishi vya wakati ujao ni a-….-ku-…..-a. Hata hivyo katika kazi yake hajagusia lolote kuhusu athari za kifonolojia zinazojitokeza wakati wa ujitokezaji wa njeo hizo. Mbali na mambo mengine lugha hizo za Kibantu zilizofanyiwa uchunguzi zinaonekana kufanana kwa kiasi fulani kiambishi cha wakati uliopita ambacho ni -ile, kwa mfano, lugha ya Kinyakyusa (Lusekelo, 2007), Kihehe (Mpalanzi, 2010) na Kindengereko (Zuberi, 2013). Pamoja na kufanana huko, imebainika pia kuwa katika lugha ya Kihehe kiambishi cha wakati uliopita kinaweza kujitokeza kwa namna tofauti tofauti kama -e-….-é, -ilé, na -ité, kulingana na kitenzi. Tazama mifano ifuatayo katika Mpalanzi (2010:60):

| Kihehe | Maana katika Kiswahili |
|---|---|
| (a) *Tu-e-tu-tof-ilé pamuvango* | (a) Tulipigana hapo zamani za kale |
| (b) *Tu-a-deny-ité* | (b) Tulivunja |
| (c) *Tu-a-tambik-é pawana* | (c) Tulitambika wakati wa utoto |

Mifano hiyo hapo juu inaonesha kuwa katika Kihehe njeo ya wakati uliopita inawakilishwa kwa viambishi vitatu yaani, -ilé, -ité, na -é.

Aidha, Nyinondi (2013) anaonesha kuwa katika Kilugulu njeo ya wakati uliopo inawakilishwa kwa kiambishi -ø- kwa maana ya kwamba hakuna kiambishi maalumu kinachoonesha njeo hiyo, kwa mfano *k-o-ghul-a* 'ananunua' ilihali njeo ya wakati uliopita inawakilishwa kwa kiambishi -tsaa kwa mfano, *-tsaa-ka-lim-a* 'alilima'. Kiambishi -tso- huwakilisha njeo ya wakati ujao kwa mfano katika kitenzi *ka-tso-ghul-a* 'atanunua'. Katika mifano hiyo tunaona kuwa wakati lugha ya Kinyakyusa, Kihehe na Kindengereko zinatumia kiambishi -ile kuwakilisha njeo ya wakati uliopita, Kilugulu hutumia kiambishi -tsaa. Tofauti hizo ni za kawaida kwa sababu pamoja na kwamba lugha zina sifa majumui kuna baadhi ya sifa ambazo ni za kipekee. Hii ina maana kwamba sifa zinazojitokeza katika lugha fulani si lazima zipatikane katika lugha nyingine kwa namna ileile. Kwa mfano, Dahl (1985), Besha (1989) na Mreta (1998) wanasema kuwa si vema kutoa kauli jumuishi kuhusu sifa za kiisimu za Kibantu kwa sababu kila lugha ya Kibantu ina sifa za kipekee pamoja na kwamba zipo katika kundi moja linalojulikana kama lugha za Kibantu. Sehemu inayofuata inajadili viambishi njeo katika Shimalila.

## 2.0 Viambishi Njeo katika Shimalila

Lugha ya Shimalila kama zilivyo lugha nyingine ulimwenguni ina aina mbalimbali za maneno kama nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihisishi na vihusishi. Makala yetu imejikita katika aina moja tu ya kategoria ambayo ni vitenzi hususani kuhusu viambishi njeo. Hii haina maana ya kwamba aina hii ya kiambishi ndiyo mtambuka katika orodha ya viambishi vyote vilivyopo katika vitenzi vya lugha hii. La hasha! Makala hii ni sehemu ndogo tu ya utafiti wa kiisimu wa lugha hii ya Shimalila. Viambishi njeo hivyo vipo vya aina tatu: viambishi njeo vya wakati uliopo, wakati uliopita, na wakati ujao, kama ambavyo ufafanuzi wake unavyoonekana katika sehemu inayofuata:

### 2.1 Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopo katika Lugha ya Shimalila

Waihiga (2010:118) anaeleza kuwa katika lugha ya Kiswahili, njeo ya wakati uliopo huwakilishwa na kiambishi '-na-'. Njeo hii huonesha kuwa kitendo kinaendelea kutendeka wakati wa kutolewa taarifa. Data ifuatayo inaonesha mfano wa njeo ya wakati uliopo katika lugha ya Shimalila. Kiambishi kinachoonesha njeo ya wakati uliopo kimekozwa. Ingawa nia ya makala hii ni kujadili njeo za

Shimalila, ufafanuzi wa dhana husika inayojadiliwa umeanza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu maana za njeo husika kama nilivyoeleza awali kuwa wanazuoni wengi wamefafanua kwa kina katika lugha ya Kiswahili tofauti na ilivyo katika lugha ya Shimalila. Hivyo, ufafanuzi huu utamsaidia msomaji kuelewa kile kinachofafanuliwa katika lugha ya Shimalila. Makala hii hailengi kulinganisha bali inaonesha namna viambishi njeo vinavyojibainisha katika Shimalila, Kiswahili kimetumika kwa lengo la kutoa fasili juu ya kitenzi kinachojadiliwa.

**Mfano wa 2:**

| Shina asili la kitenzi | Kiambishi cha wakati uliopo | Fasiri yake katika Kiswahili |
|---|---|---|
| *yinga* | *a-**ku**-yinga* | 'anatetemeka' |
| *gana* | *a-**ku**-gana* | 'anapenda' |
| *siibha* | *a-**ku**-siibha* | 'anawaza' |
| *manya* | *a-**ku**-manya* | 'anafahamu/anajua' |
| *sambila* | *a-**ku**-sambila* | 'anasoma |
| *gwa* | ***a-ku**-gwa* | 'anaanguka' |
| *sya* | *a-**ku**-sya* | 'anasaga' |
| *lya* | *a-**ku**-lya* | 'anakula' |
| *swa* | *a-**ku**-swa* | 'anatema' |
| *fwa* | *a-**ku**-fwa* | 'anakufa' |

Data iliyopo hapo juu inaonesha kuwa katika lugha ya Shimalila kiambishi cha njeo ya wakati uliopo kinawakilishwa kwa kutumia kiambishi **-ku-**'. Kiambishi hiki kinatokea baada ya kiambishi cha nafsi ya kwanza '-a-'. Kwa mfano katika kitenzi *sya* 'a-**ku**-sya' na kitenzi *gwa* 'a-**ku**-gwa'.

## 2.2 Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopita katika Shimalila

Waihiga (2010) anaeleza kuwa katika lugha ya Kiswahili njeo ya wakati uliopita huwakilishwa na kiambishi '-li-'. Njeo hii huonesha kuwa kitendo kilitendeka kabla ya kutolewa kwa habari. Katika lugha ya Shimalila kiambishi njeo huwakilishwa na kiambishi '-il-'. Ifuatayo ni data inayoonesha njeo ya wakati uliopita katika lugha ya Shimalila:

**Mfano wa 3:**

| Shina asili la kitenzi | Kiambishi cha wakati uliopita | Fasiri yake katika Kiswahili |
|---|---|---|
| *yinga* | *áyinj-**il**-e* | 'alitetemeka' |
| *gana* | *ágan-**il**-e* | 'alipenda' |
| *siibha* | *ásibh-**il**-e* | 'aliwaza' |
| *manya* | *ámany-**il**-e* | 'alifahamu/alijua' |

| | | |
|---|---|---|
| *pinya* | *ápiny-**il**-e* | ‘alifunga’ |
| *gwa* | *ágw-**iy**-e* | ‘alianguka’ |
| *sya* | *ás-**iy**-e* | ‘alisaga’ |
| *lya* | *á**l-iy**-e* | ‘alikula’ |
| *swa* | *ásw-**iy**-e* | ‘alitema’ |
| *fwa* | *áfw-**iy**-e* | ‘alikufa’ |

Data katika mfano wa 3 hapo juu inaonesha kuwa katika lugha ya Shimalila kuna viambishi vya aina mbili vinavyoonesha njeo ya wakati uliopita. Yaani, kiambishi ‘-il-’, na kiambishi ‘-iy-’. Ujitokezaji huu ni tofauti na namna ilivyo katika lugha ya Kiswahili kwa sababu katika Kiswahili Sanifu njeo ya wakati uliopita huwakilishwa na kiambishi njeo ‘-li-’ ilhali katika lugha ya Shimalila kuna kiambishi ‘-il-’ na ‘-iy-’. Kiambishi njeo ‘-il-’ cha njeo ya wakati uliopita katika Shimalila hujitokeza katika vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja wakati kiambishi njeo ‘–iy- hujitokeza katika vitenzi vyenye silabi moja kama mifano inavyojidhihirisha katika mfano wa tatu. Aidha, katika lugha ya Shimalila kiambishi njeo kinajitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Vilevile katika lugha ya Shimalila viambishi vya njeo ya wakati uliopita vinaonekana kuwa ni viambishi unganishi kwa maana ya kwamba ni vile viambishi vilivyoundwa kwa silabi mbili yaani $i$ na $l$, pia $i$ na $y$. Hii ni tofauti na ilivyo katika lugha ya Kiswahili ambapo kiambishi cha njeo ya wakati uliopita kinaundwa na silabi moja tu ambayo ni $li$.

Aidha, data hiyo inaonesha kuwa mabadiliko ya njeo yanategemea aina ya kitenzi kinachohusika. Ikiwa kitenzi ni kile kisoukomo na chenye umbo la silabi zaidi ya moja kiambishi kinachoambikwa katika kitenzi hicho ni kiambishi ‘**-ile-**’. Hali kadhalika data inaonesha kuwa kama kitenzi kina umbo la silabi moja kiambishi cha njeo kinachopachikwa ni kiambishi ‘**-iye-**’ kama mifano inavyodhihirisha. Aidha, data inaonesha kuwa katika Shimalila kiambishi njeo cha wakati uliopita kinapopachikwa katika umbo la kitenzi kiambishi tamati ‘–a’ hubadilika na kuwa ‘-e’. Pia, utafiti unaonesha kuwa mabadiliko haya hayajitokezi katika kiambishi cha njeo ya wakati uliopo kwa sababu katika vitenzi vyenye shina la silabi zaidi ya moja na vile vyenye shina la silabi moja, kiambishi njeo kinabaki kilekile yaani ‘-ku-’.

Pia, kuna mabadiliko mengine yanayojitokeza. Mabadiliko hayo yanahusisha kubadilika kwa konsonanti ya mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Aidha, mabadiliko hayo yanasababishwa na uambikwaji wa kiambishi njeo cha wakati uliopita katika mzizi wa kitenzi. Hebu tazama mifano ifuatayo katika data inayofuata:

**Mfano wa 4:**

| Shina asili la kitenzi | Kiambishi cha wakati uliopita | Fasiri yake katika Kiswahili |
|---|---|---|
| *liga* | *álij-**il-e*** | 'alitukana' |
| *yeega* | *áyeej-**il-e*** | 'alioa' |
| *ega* | *áyej-**il-e*** | 'alioa' |
| *lega* | *álej-**il-e*** | 'alikwepa' |
| *yinga* | *áyinj-**il-e*** | 'alitetemeka' |

Data iliyopo hapo juu inaonesha kuwa kuna mabadiliko ya konsonanti mwishoni mwa mzizi wa kitenzi mara baada ya uambikaji wa kiambishi cha njeo katika mzizi wa kitenzi. Kwa mfano, konsonanti /g/ ambayo ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini inabadilika na kuwa /ɟ/ ambayo ni kikwamizi ghuna cha kaakaa gumu. Hali hii inadhihirisha kuwa katika lugha ya Shimalila mchakato wa kuambika viambishi awali katika vitenzi mathalani kiambishi njeo cha wakati uliopita unahusisha taaluma mbili za kiisimu, yaani taaluma ya mofolojia na fonolojia. Hapa ina maana ya kwamba wakati wa upachikaji wa viambishi njeo katika lugha ya Shimalila kuna mabadiliko ya sauti yanayojitokeza kutokana na sababu za kiisimu. Mabadiliko hayo hayawezi kuelezwa kwa sababu za kimofolojia tu kwa vile yanahusu kubadilika kwa sauti suala ambalo ni la kifonolojia, taaluma inayohusu uchambuzi wa sauti za lugha mahsusi.

Mbali na mambo mengine, katika lugha ya Shimalila upachikaji wa kiambishi njeo cha wakati uliopita unakwenda sambamba na mabadiliko ya toni katika kiambishi cha nafsi kilichopo katika kitenzi husika. Hali hii ni tofauti na ilivyo katika hali iliyopita timilifu ambapo toni inayohusika ni toni chini[2]. Hata hivyo suala la toni katika lugha hii linahitaji uchunguzi wa kina. Sehemu inayofuata inahusu kiambishi njeo cha wakati ujao katika Shimalila.

## 2.3 Kiambishi Njeo cha Wakati Ujao katika Lugha ya Shimalila

Waihiga (2010:119) anasema kuwa kiambishi cha njeo ya wakati ujao huonesha kuwa kitendo bado hakijatendeka lakini kinatarajiwa kutendeka baadaye. Njeo hii huwakilishwa na kiambishi '-ta-' katika lugha ya Kiswahili. Lifuatalo ni jedwali linaloonesha ujitokezaji wa kiambishi njeo cha wakati ujao katika Shimalila.

**Mfano wa 5:**

| Shina asili la kitenzi | Kiambishi cha wakati uliopita | Fasiri yake katika Kiswahili |
|---|---|---|
| *yinga* | *a-**ti**-yinje* | 'atatetemeka' |

[2] Kwa ufafanuzi zaidi tazama mfano wa 6 katika ukurasa unaofuata.

| | | |
|---|---|---|
| *duga* | *a-**ti**-duje* | 'atarudi' |
| *ega* | *a-**ti**-yeje* | 'atachukua' |
| *yeega* | *a-**ti**-yeeje* | 'ataoa' |
| *lega* | *a-**ti**-leje* | 'atakwepa' |
| *liga* | *a-**ti**-lije* | 'atatukana' |
| *gana* | *a-**ti**-gane* | 'atapenda' |
| *siibha* | *a-**ti**-sibhe* | 'atawaza' |
| *manya* | *a-**ti**-manye* | 'atafahamu/atajua' |
| *sambila* | *a-**ti**-sambile* | 'atasoma' |
| *gwa* | *a-**ti**-gwe* | 'ataanguka' |
| *sya* | *a-**ti**-sye* | 'atasaga' |
| *lya* | *a-**ti**-lye* | 'atakula' |
| *swa* | *a-**ti**-swe* | 'atatema' |
| *fwa* | *a-**ti**-fwe* | 'atakufa' |

Data hiyo hapo juu inaonesha kuwa katika lugha ya Shimalila kiambishi njeo cha wakati ujao kinawakilishwa kwa kiambishi '-ti-'. Aidha, uambikaji wa kiambishi cha njeo ya wakati ujao kama ilivyo katika njeo ya wakati uliopita unaelekea kuambatana na mabadiliko ya baadhi ya sauti {fonolojia}. Kwa mfano, katika kitenzi 'yeega' (*oa*),' wakati ujao ni 'atiyeeje' (*ataoa*). Tukiangalia katika mfano huu mzizi wa kitenzi ambacho hakijafanyiwa mchakato wowote ni 'yeeg-', wakati mzizi uliofanyiwa mchakato wa uambatizi ni 'yeej-. Hivyo basi, konsonanti /g/ ambayo ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini imebadilika na kuwa konsonanti /ɟ/ ambayo ni kipasuo kwamizi cha kaakaa gumu. Mabadiliko haya yametokana na uambatizi wa kiambishi njeo cha wakati ujao. Pia kuna nduni nyingine zinazojitokeza katika data. Data za makala hii zinaonesha kuwa kiambishi tamati maana cha shina la kitenzi ambacho hakijaambishwa ni '-a' lakini baada ya kuambishwa kiambishi njeo ya wakati uliopita na ujao kiambishi tamati maana cha kitenzi katika Shimalila kinabadilika na kuwa '-e.' Sababu za mabadiliko hayo zinaonesha ni tabia asilia ya vitenzi vya lugha hiyo hususani baada ya kufanyika kwa mchakato wa uambatizi.

Pamoja na uambikwaji wa viambishi njeo ya wakati ujao kusababisha mabadiliko ya kifonolojia ya baadhi ya sauti kama ilivyoelezwa hapo juu. Data zinaonesha kwamba katika baadhi ya vitenzi vyenye mofolojia sawa na vile vinavyobadilika havibadiliki. Kwa mfano, kitenzi **gwa** 'anguka' kikiwa na kiambishi njeo *ati**g**we*, *gana* 'penda' *ati**g**ane* 'atapenda'. Katika mifano hii hakuna mabadiliko ya sauti /g/ katika kitenzi kisoukomo na sauti /g/ iliyopo katika kitenzi kilichoambikwa kiambishi njeo ya wakati ujayo. Ujitokezaji huo ni tofauti na ilivyo katika vitenzi vingine vilivyobainishwa katika mfano wa 5 hapo juu.

Si lengo la makala hii kujadili suala la viambishi hali mathalani kiambishi cha wakati uliopita timilifu katika lugha ya Shimalila. Hata hivyo tumeona tugusie walau kwa ufupi hali hiyo kwa lengo la kuonesha namna maumbo ya kiambishi cha njeo ya wakati uliopita na kiambishi cha njeo ya wakati uliopita timilifu yanavyoathiriana kimofolojia, kifonlojia, na kisemantiki. Ifuatayo ni data inayoonesha njeo ya wakati uliopita timilifu:

**Mfano wa 6:**

| **Shina asilia la kitenzi** | **Fasiri yake katika Kiswahili** | **Kiambishi cha njeo iliyopita timilifu** | **Fasiri yake katika Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| *yinga* | tetemeka | *à-yinj-**il**-e* | 'ametetemeka' |
| *gana* | penda | *à-gan-**il**-e* | 'amependa' |
| *siibha* | waza/fikiri | *à-siibh-**il**-e* | 'amefikiria' |
| *manya* | fahamu/jua | *à-many-**il**-e* | 'amejua' |
| *pinya* | funga | *à-piny-**il**-e* | 'amefunga' |
| *gwa* | anguka | *à-gw-**iy**-e* | 'ameanguka' |
| *sya* | saga | *à-sy-**iy**-e* | 'amesaga' |
| *lya* | la | *à-l-**iy**-e* | 'amekula' |
| *swa* | tema | *à-sw-**iy**-e* | 'ametema' |
| *fwa* | fa | *à-fw-**iy**-e* | 'amekufa' |
| *yeega* | oa | *à-yeej-il-e* | 'ameoa' |
| *ega* | chukua | *à-yej-**il**-e* | 'amechukua' |
| *lega* | kwepa | *à-lej-**il**-e* | 'amekwepa' |
| *liga* | tukana | *à-lij-**il**-e* | 'ametukana' |

Data katika mfano wa 6 hapo juu inaonesha kuwa katika lugha ya Shimalila hakuna tofauti ya kimofolojia baina ya kiambishi cha njeo ya wakati uliopita na kile cha wakati uliopita timilifu yaani kiambishi '-il- na –iy- hutumika kurejelea njeo ya wakati uliopita pia hurejelea wakati uliopita timilifu tofauti na ilivyo katika lugha ya Kiswahili ambapo kiambishi '-li-' hutumika kurejelea njeo ya wakati uliopita ilhali kiambishi '–me-' hutumika kurejelea wakati uliopita timilifu[3]. Pia, hakuna utofauti wa kimofolojia wa viambishi hivyo yaani kiambishi cha wakati uliopita na ule uliopita timilifu kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi cha wakati uliopita ni '-li-' na kiambishi cha wakati uliopita timilifu ni '-me-'. Makala yetu inaonesha kuwa katika lugha ya Shimalila viambishi vinavyoonesha njeo ya wakati uliopita ni '-il-' na '–iy-'; kwa mfano, katika vitenzi *yinga* 'a-yinj-**il-**e' na katika kitenzi *fwa* 'a-fw-**iy**-e'.

[3] Ieleweke kuwa si lengo la makala hii kujadili kiambishi hicho cha hali bali hapa kimetumika tu kama kichokoo cha kuonesha uhusiano uliopo baina ya njeo iliyopita na kiambishi njeo ya wakati uliopita timilifu.

Aidha, data zinaoneshakuwa unaweza kutofautisha njeo iliyopita na iliyopita timilifu kifonolojia na kisemantiki. Tunaposema kifonolojia tuna maana ya kwamba kiambishi cha nafsi kinapopachikwa kwenye mzizi wa kitenzi na kuwa na toni juu basi njeo inayojidhihirisha ni ya wakati uliopita. Kiambishi cha nafsi kinapopachikwa kwenye umbo kitenzi lenye kiambishi njeo ya wakati uliopita kinapokuwa na toni chini basi njeo inayojidhihirisha ni ya wakati uliopita timilifu. Kama tulivyosema awali kuwa tunazungumzia kwa ufupi kipengele cha kiambishi cha njeo ya wakati uliopita timilifu. Utafiti zaidi unahitajika kuhusu ujitokezaji wa namna hali inavyojibainisha katika Shimalila ikiwa ni pamoja na uhusiano wake na njeo.

**3.0 Hitimisho**

Makala hii imejadili kuhusu ujitokezaji wa viambishi vya njeo katika lugha ya Shimalila. Katika kujadili ujitokezaji huo imebainika kuwa katika lugha ya Shimalila viambishi vya njeo hujitokeza kwa namna ya pekee sana tofauti na ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Shimalila njeo ya wakati uliopo huwakilishwa kwa kiambishi '-ku-' wakati njeo ya wakati ujao huwakilishwa na kiambishi '-ti-' ilhali njeo ya wakati uliopita huwakilishwa na viambishi viwili yaani kiambishi '-il-' na '-iy-'. Vilevile tumeona kuwa upachikaji wa viambishi njeo katika lugha ya Shimalila huweza kuathiriwa na sababu za kifonolojia kwa mfano katika mfano wa 3 na wa 4 data inaonesha kuwa katika baadhi ya vitenzi konsonanti ya mwisho wa mzizi hubadilika baada ya upachikaji wa viambishi njeo vya wakati uliopita na wakati ujao. Hali kadhalika, tumeona kwamba kimofolojia hakuna utofauti uliopo kati ya njeo ya wakati uliopita na ile ya wakati uliopita timilifu.

Kifonolojia tofauti kati ya njeo iliyopita na njeo iliyopita timilifu ipo na inajibainisha kwa toni juu na toni chini kuwekwa katika kiambishi cha nafsi (mtenda). Pia, tumegundua kuwa kuna utofauti wa mazingira ya utokeaji wa viambishi njeo katika Shimalila. Hii ina maana kuwa kuna baadhi ya viambishi njeo kama vile vya wakati uliopo na vya wakati ujao vinajitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi ilhali viambishi vya njeo ya wakati uliopita na vile vya wakati uliopita timilifu vinajitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Ujitokezaji huu unaleta udadisi na kutufanya tujiulize baadhi ya maswali ambayo yanatusaidia kutokuwa na fikra jumuishi za kudai kuwa katika lugha za Kibantu viambishi vya wakati hujitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi. Tunatakiwa kufanya utafiti wa lugha nyingi kadri itakavyowezekana ili tujue ni lugha zipi viambishi njeo vyake hujitokeza kabla ya mzizi na zipi viambishi njeo vyake hujitokeza baada ya mzizi. Hata hivyo kusudi la makala hii ni kuibua uchochezi wa utafiti zaidi wa suala la viambishi njeo na viambishi vingine katika Shimalila na lugha nyingine za Kibantu ambazo hazijafanyiwa utafiti katika uwanja huu.

## Marejeleo

Besha, R. M. (1989). *A Study of Aspect, Tense and Action*. Berlin: Dietrich Reimer Verlag.

Chomi, E. W. (2001). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Sebha: African Studies Research Centre.

Chomi, E. W. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Cosmas, C.N. (2010). Tense and Aspect Systems in Kihangaza. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Dahl, Ö. (1985). *Tense and Aspect Systems*. New York: Basil Blackwell Inc.

Habwe, J. na Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Julius, M. na wenzake (2009). *Ishitaabu isha Tupango utwa Shimalila*. Mbeya: SIL Internatonal. Julius, M. (Mfasiri) (2009). *Uyeesu Akumuzyusya Umwana wa Mwantanda Umufwile*. Mbeya: Huduma ya Kutafsiri Biblia na Kuendeleza Lugha za Asili katika Mkoa wa Mbeya na Iringa.

Kanijo, P. (2012). Formatives of Tense and Aspect in the Verbal Construction Kinyamwezi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lusekelo, A. (2007). Tense and Aspect Systems in Kinyakyusa. Tasnifu ya Umahiri, (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba na wenzake (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Mbeyale, R. na wenzake (2001). Tukithamini Kimalila. Mbeya: Huduma ya Kutafsiri Biblia na Kuendeleza Lugha za Asili katika Mkoa wa Mbeya na Iringa.

Mdee, J. S. (2007). *Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Loghorn Publishers.

Mpalanzi, L. (2010). An Analysis of Tense and Aspect System in Kihehe: A Case of Affirmative and Negative Constructions: Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mreta, A.Y. (1998). An Analysis of Tense and Aspect in Chasu: Their forms and Meaning in the Affirmative Constructions. Hamburg: LIT.

Muzale, H.R.T. (1998). A Reconstruction of the Proto-Rutara Tense / Aspect Systems Linguistics, Tasnifu ya Uzamivu, (haijachapishwa). Newfoundland Univerisity.

Nurse, D. (2003). "Aspect and Tense in Bantu Languages", In Nurse, Derek and

Gérard Phillipson (wah.) *The Bantu Languages*. London: Routledge, uk. 517-544.

Nkwera, F. V. (2003). *Sarufi Fasihi na Uandishi wa Vitabu Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nyinondi, O. (2013). Tense and Aspect in Luguru, Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Waihiga, G. (2010). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publisher.